

Tarehe 05.04.2024

**TANGAZO LA ZABUNI YA MACHAPISHO YA VITABU/HATI KWA MATUMIZI YA OFISI
MSIMU 2024/2025**

Zabuni na: KCU/Z/2024/2025/04

1. KCU (1990) LTD imetenga fedha kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kimkataba na mtoa huduma ya Uchapishaji vitabu/hati kwa msimu 2024/2025.
2. Makampuni/Mtu binafsi yanayotambulika yanakaribishwa kuleta maombi ya zabuni hii ili kutoa huduma ya Uchapishaji vitabu/hati kwa msimu 2024/2025.
3. Mwombaji awe na leseni ya biashara pamoja na TIN/VAT.
4. Mwombaji ataje utaratibu wake wa kupata malipo yake.
5. Ombi la zabuni liwe na jina, anuani halisi la mwombaji na mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
16. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kuitia A/C Namba **01J1055955001 KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LTD** iliyopo CRDB
6. Mwombaji afike katika ofisi ya manunuzi kwa ajili ya kupewa orodha ya vitabu vitakavyochapishwa.
7. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 1-7 vilivyo tajwa hapo juu.
8. Barua za maombi zilizofungwa katika bahasha yenye lakiri na kuandikwa juu yake:-
“MAOMBI YA ZABUNI YA MACHAPISHO YA VITABU/HATI KWA MATUMIZI YA OFISI MSIMU 2024/2025” kwa anuani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.

9. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika ofisi ya manunuzi KCU (1990) Ltd kabla au mnamo tarehe 19.04.2024. saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni
10. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.

Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

